MCHEZO WA KUIGIZA KUHUSU UGONJWA WA UKIMWI

Intertwining Lives

WAIGIZAJI

Alex : mtoto wa Peter na Helen
Graham : Rafiki ya Tina
Helen : Bibi ya Peter
Jayne : Mshauri
Julie : Muuguzi
Peter : Bwana ya Jane
Tina : Mpenzi wa Peter

WAIGIZAJI WENGINE

Muuzaji Pombe
Mhudumu wa hoteli
Muuguzi

ONYESHO LA KWANZA

Lafanyika kwenye jikoni kwa nyumba mmoja mtaani.Helen amesimama kwa mfereji anaosha majani ya ku;a usiku.Helen ni mja mzito .Bwana yake Peter amekaa mezani anasoma gazeti. Kabuti lake liko juu ya kiti na mkoba wake uko juu ya meza.Ingawaje Peter na Helen wamenyamaza lakini kuna sauti za mtoto mdogo ambaye anacheza na kucheka.Helen ana maliza kuosha majani na kuziweka kwenye bakuli kisha amamwangalia mumewe na ananza kuongea :

Helen. Hujasema mengi.

Peter [anawacha kusoma gazeti]. Sina mengi la kusema, ni vile niko na kazi mingi ya kufanya. **[anaendelea kusoma gazeti]**

Helen. Nime ona hivyo.siku hizi haukuji nyumbani .**[ananyamaza]** hatuonani kabisa siku hizi.

Peter [Bado ana soma gazeti] Pole nini?

Helen [Anaongea kwa sauti] Nime sema hatuonani kabisa siku hizi.

Peter [Anahema ,ana kunja gazeti na kusimama] Na jua mpenzi, najua. Ni vile kuna kazi mingi sana ya kufanya hivi sasa , kazi ikiisha nita kuwa nyumbani. **[Anamwekelea Helen mkono mabegani]**

Helen [Anawekelea kicwa kwenye kifua cha Peter] lakini utamaliza lini?ni kama kila wakati ukimaliza kazi moja wanakupatia kazi nyingine.Nasi mimi pekee yangu unafaiwa kumfikiria Alex unajua kila siku ananiuliza kule uko na utakuja saa ngapi na sijui ni mjibu aje. **[Anainua kichwa na kumwangalia Peter]** yeye huwa amelala wakati unakuja.usiku ni ngumu sana kwake kuelewa na ni ngumu sana kwangu kumueleza.Utafanya nini wakati huyu atazaliwa**[Anashika tumbo]** na wote wananiuliza juu yako?

Peter [Anamwachilia na sauti yake inakuwa kali] Sijui unataka ni seme nini mpenzi . Siwezi kuwa kila mahali ..nyumbani na kazini! Siku moja Alex ataelewa ninafanya kazi ili aishi maisha nzuri ,shule yake haijilipiunajua. **[Helen anaanza kukasirika na Peter anaongea kwa upole]** Vitu ni ngumu kwangu pia. Unaonaji tukae pamoja hii wikendi?Tunaweza kwenda kwenye uwanja?labda tunaweza kwenda kuona wanyama najua Alex atapenda hivyo.

Helen. [Anatabasamu] Maajabu!Alex atafurahia.

[Anasita.Na simu ya mkono ina lia.]

Peter Pole mpenzi wacha nishike simu . **[Anatoa simu kwenye mfuko wa kabuti]** Jambo?sawa nakuja hivi sasa , najua siwezi kosa sawa , tuonane.

Helen. Kazi tena !

Peter [Anavaa kabuti na kuondoka] Sawa pole mpenzi. Wananitaka kazini nimalize kazi fulani labda watanipandisha cheo na wataniongezea pesa.**[Helen anambusu]**

Helen. Nita kuwa nimelala wakati utakuja.

Peter. Sitakuamsha**[Anaondoka]**

Helen. [Anaangalia mimba yake] Hatahakuuliza juu yako **[Anachukua majani na kuanza kukatakata]**

ONYESHO LA PILI

La fanyika kwa baa.Kuna kelele ya musiki na mataa yanawaka kila mahali na watu wanakunywa pombe na kucheza.Kwenye meza kuna mwanamke mrembo ambaye ana kunywa pombe na anangonja mtu.Anafungua mfuko na kutoa kioo na rangi ya mdomo na anaanza kupaka.Anaangalia mlango.

Muuzaji pombe: Aja kusahau ?
Tina. Hapana! mimi si wezi kusahaulika.

[Anaangalia mlango na anaingia, amebeba mkoba wake.Anaangalia baa anamuona

na kwenda kwake]

Tina. [kwa muuzaji pombe] nilikuambia**[Peter anakuja]** habari mpenzi mbona umechukua muda mrefu**[Wanabusu].** kwa kawaida unakujanga kwa haraka.

Peter. Nilikuwa nikihojiwa lakini niko hapa sasa.

Tina. Bibi yako alikuwa anakuuliza maswali? ulimwambia unafanya kazi usiku?Huyo mwanamke hajui kitu kama ni mimi ningekuwa nimejua.

Peter. Oh ndio? basi ni bahati si wewe kwasababu yeey hajui.Anafikiria nina fanya kazi li niwezee kusaidia familia yangu.**[Anamshika nywele na mguu]** na hata kama tutashikwa nisawa . **[Wanabusu]** tunaenda kwako?

Tina [Anacheka] Mpenzi hakuna kitu kingine unafikiria?

Peter. Niseme nini ? si pendi kupoteza wakati ,kila mtu huniambia hivyo kazini.

Tina [Anacheka na kuchukua mfuko wake] Sawa basi twende kwangu. Hatuwezi kwenda kwako?!

Peter anamwekelea mkono mabegani na wanaondoka.

ONYESHO LA TATU
Lafanyika kwenye nyumba lakuishi. Peter na Tina wamekaa kwa sofa wakibusu .Koti la Peter liko juu ya kiti na nkoba wake uko kwa simiti. Wote wametoa nguo za juu na Peter hana shati lake na shati la Tina limefunguliwa mfuko wake uko chini kando ya sofa.

Tina.[anawacha kumbusu Peter na anachukua mkoba wake na kutoa kondomu]. Tunaweza kuendelea kwenye chumba cha kulala?

Peter. Sawa. **[Anaona kondomu].** hiyo ni ya nini?

Tina. Mpenzi nadhani ni vizuri kujichunga .si taki kupata mimba au kitu kingine.

Peter. Nilidhani unameza madawa ya kupanga uzazi.

Tina. Najua lakini kuna vitu zingine isipokuwa mimba. kama ugonjwa nadhani tunafaa kuji chunga.

Peter. Ngoja. kwanini tujichunge ugonjwa ,,, nimekuwa nikilala na wewe na Helen pekee kwani umekuwa na mwanamume mwingine?

Tina. [Anaangalia chini kwa dakika] Hapana! lakini nimekuwa na wanaume wengine

zamani na pia wewe sisi si malaika na pia sijawai pimwa ,wewe umepimwa?

Peter. Hapana , lakini sitaki kupimwa na pia wewe.**[Anambusu na kutoa kondomu kwa mkono].** mpenzi tumekuwa tukifanya mapenzi bla kutumia kondomu kwa miezi miwili _ kama ugonjwa ilikuwa itushike tayari tungekuwa nayo.pia kondomu haina raha .

Tina [Kwa wasiwasi] Sawa…natumekuwa tukifanya kwa miezi, na si dhani nikomgonjwa sisikii vibayana ni raha bila kondomu …**[Peter anaanza kumbusu]**
Peter [Anawacha kumbusu anatupa kondomu kwa sofa na kumshika mkono na kumuamsha]. Ndio mpenzi nadhani tumepoteza wakati wa kutosha tayari ... **[Wanaenda kwenye chumba cha kulala]**

ONYESHO LA NNE

Miezi kadhaa zimepita .Tina yuko nyumbani kwake. Simu inalia

Tina. Habari? **[Anakunja uso kwani hajui sauti ni ya nani]** Graham ?Habari yako ?**[Anatingisha kichwa]**
Sijakuona kwa muda mrefu!Tunafaa kukutana . Tukutane lini?**[Anasita]** sawa tukutane leo mchana ??**[Anasita]** Graham uko sawa? Unaongea ...sijui... **[Anasita]** sawa tukutane wapi ?Kahawa huko Al Fresco kama saa kumi na moja **[Anasita]** sawa tukutane huko.

ONYESHO LA TANO

lafanyika mkahawa wa Al fresco.Graham amekaa kwa meza pekee yake anaangalia kando na kuangalia kinywaji chake.Tina anaingia na Graham anasimama kumsalimia.

Tina. Habari Graham !**[Ana Kumbatia]** Nivizuri kukuona ! nilikuona lini mwisho?

Graham. Kama miezi tatu au nne. **[Wana kaa chini.]**

Tina [kwa mhudumu wa hoteli] Niletee kahawa? **[kwa Graham]** umekuwa ukifanya nin wakati huu wote? Mwisho nilikuona siku ya krismasi ulikuwa unasafiri ?

Graham [bila starehe] ndio **[anasita]** nilirudi tena unajua, Indonesia ,Thailand, India…Nilikutana na watu wengi ....nime pata marafiki wengi.

[Mhudumu wa hoteli ana rudi na kahawa ya Tina]

Tina [Akimchezea] ulikutana na mtu yeyote?

Graham [bila starehe] hapana kwa nini?

Tina Najua…basi hatungekuwa pamoja siku ya krismasi.

Graham [Anakohoa] Tina lazima tuongee kuhusu hiyo siku , niko na habari mbaya.

Tina. Nini?

Graham. Nikisafiri nili lala na watu kidogo ...na wengi wao walikuwa wasafiri na sikudhania sana juu yao , unajua?

Tina. Unasema nini?

Graham. Niliporudi nyumbani nilienda kpimwa ugonjwa wa zinaa ili kuhakikisha niko sawa na nili patikana na chlamydia.

Tina [Anachanganikiwa] Graham, Mbona unaniambia?

Graham [Anaangalia kinywaji chake] kwa sababu unaweza kuwa ulipata ....na hiyo siku ya krismasi hatukutumia kitu . Na unaweza kuwa nayo na pia pia mtu yeyote umelala naye kutoka hiyo siku **[anasita]** unaona mtu yeyote?

Tina [flustered]. niliona kama watu wawili ,,,, naona wanaume wawili kwa hivi sasa.

Graham . Pole Tina lakini unafaiwa kujua. Jaribu kwenda kutibiwa.... wana tibu chlamydia kwa haraka na ni muhimu uambie mwanamume yeyote ambaye umelala naye.

Tina. Nilazima niwaambie?

Graham Ndio ni lazima uwaambie– kwasababu isipotibiwa inaweza kuwa mbaya sana ...kama hutaki kuwaambia aunaweza kumwambia daktari ama muuguzi awaambie na asiseme jina lako.[anasimama] sikia pole sana kwa kukuambia habari mbaya , pole wacha niende.

Graham anaenda . Tina ana wachwa pekee yake kwa hoteli.

ONYESHO LA SITA

Lafanyika kwa kliniki ya GUM. Tina amekaa mahali pa wagonjwa na hana starehe , ako na gazeti kwa mapaja lakini hasomi .Muuguzi anaingia.

Nurse Tina Barrett tafadhali!

Tina anasimama na kuingia mahali pa wagonjwa kuonekana.

Julie. Habari Tina mimi ni Julie , muuguzi wa kufundisha watu juu ya ngono.. Nitakuuliza maswali kuhusu maisha yako na ningependa unijibu kwa ukweli ili tujue tukupime nini? sawa?

Tina. Sawa

Julie. Sawa .Tina uko na mpenzi mmoja, ama unafanya mapenzi na zaidi ya mtu moja.

Tina. Umm... niko na wote.Niko na mpenzi mmoja wa kawaida lakini si yeye pekee yake**[anasita]** unaona nililala na mwanamume mwingine miezi mbili iliyo pita na hivi karibuni aliniambia ametibiwa chlamydia.

Julie. Na ulifanya mapenzi aina gani?

Tina. Um…Aina yote.
Julie. Ulitumia kondomu?Unatumia kondomu na wanaume hawa?

Tina . Hapana ....mimi hujaribu lakini natumia tembe kwa hivyo sifikiri sana juu ya kondomu.

Julie. Tina, ni muhimu kutumia kondomu kila wakati. kama haujichungi si mimba pekee inaweza kukushika pia magonjwa ya zinaa..magonjwa mengine ya zinaa hayajulikani mpaka mtu atibiwe . **[anasita]** ukiwa na ugonjwa wa zinaa na isitibiwe mapema ina weza lete ugonjwa kama ukimwi.Sawa nitakupima kama uko na magonjwa yoyote utanipa damu na mkojo.mkojo unapimwa chlamydia na damu kisonono na ukimwi .Tina unataka kupimwa zote au moja?

Tina. Haijalishi? si nitajua kama niko na ugonjwa wa ukimwi.

Julie. Si lazima .Virusi vinaweza kuishi mwilini kwa miaka mingi bila wewe kujua.kupimwa ugonjwa huu si mchezo na kwasababu ukimwi ni ugonjwa wa maisha na kuna uzuri na ubaya wa kujua hali yako.

Tina. Kama nini?
Julie. Uzuri ni ukipatikana uko na virusi utapata matibabu mapema na unaweza ishi maisha marefu ,madawa mapya yana tengenezwa kila wakati pia kuishi na virusi inamaanisha ujichunge kila wakati.pia unaweza panga maisha yako ya mbele kama utapata watotot au la na pia unaweza kuambia wapenzi wako ama tuweza kuwaambia kwa niaba yako.pia Tina ukipimwi na upatikane bila virusi unafaiwa kujichunga na kutumia kondomu kila wakati kumbula si lazima matokeo yatoke na virusi.

Tina. Sawa ...naona ...na ubaya wa kupimwa ni nini?

Julie. kujua hali yako inaweza kukufanya ufikirie sana. Na inalingana na vile utaikubali na pia kama uko na watu wakutegemea .Ukona marafiki wa kutegemea?

Tina. mimi na mama yangu tunasikizana na naweza kumtegemea ingawaje sijamwambia juu ya maisha yangu najua anataka nitafute bwana.

Julie. Nadhani matokeo yakionyesha uko na virusi basi unafaiwa kumweleza mama yako ili uweze kumtegemea.nimeona watu ambao wamechanganikiwa na hawaamini wako na virusi.Ni muhimu kujua hali yako kwani unafaiwa kubadilisha vitu vingi kwa maisha

yako. Itabidi pia familia yako ibadilike .

Tina. Wow, hii ni swala kubwa **{anasita}** sijui ni fanyeaje.

Julie. Usijali si lazima uharakishe majibu yako...lakini fikiria kila kitu tumeongea na ufanye vle unafikiri ni sawa kwako pia kumbuka kila kitu tunachoongea hapa ni siri na haufaiwi kujali **[anamka]** ungependa kikombe kikombe cha chai ili ufikirie kile utafanya.

[Julie anaondoka. Tina anawachwa pekee yake.]

Tina. [anafikiria] nikipimwa na nipatikane na virusi lazima niambia wapenzi wangu niko na virusi ...peter...tony...Graham..lakini si lazima niwaambie waauguzi wa hapa wanaweza kuwa ambia lakini watu watanifikiria aje?Hii ni ugonjwa ya maisha na ni lazima nimeze madawa kila siku na nimesikia mtu husikia vibaya .Nitaweza kuapata kazi ?ama nitakuwa mgonjwa sana? Na kama nataka watoto lakini naweza wapitishia virusi hivi? Nitamwambia aje mamangu?Atakasirika sana? La sitapimwa hali yangu ya ukimwi**.[anasita]** lakini kama niko nayo na sijui?nikikutana na mtu na nimpende naweza mpitishia virusi kwa sababu niliogopa kupimwa na tukiamua kupata mtoto naweza kumpitishia virusi hivi.Na hii si vizuri kwao **[anahema]** Peter ana bibi na watoto na familia.Naweza kuwa nayo **[anasita]** hata labda sina .Nitakubali kupimwa.

[Julie anarudi na kikombe cha chai]

Julie. Sawa Tina umeweza kuamua kama utapimwa leo au la?Kumbuka usiharakishe na unaweza kuja siku nyingine kupimwa tunaweza kukupimwa chlamydia na kisonono leo uko sawa na hiyo?

Tina. [anaonekana kama anaogopa] Hapana ni sawa nimefikiria na nimeona niafadhali ni pimwe hata labda sina virusi.

Julie. Uko na uhakika ? **[Tina ana tingisha kichwa]** sawa tutapima damu kwanza halafu mkojo halafu ukuje baada ya wiki moja tuongee juu ya matokeo.

Tina. Asante

ONYESHO LA SABA

<u>BAADA YA WIKI MOJA</u>

lafanyiki kwenye kliniki ya GUM. Tina amekaa mahali pa wagonjwa.

Muuguzi. Tina Barrett!
Tina anaamka na kuingia mahali pa wagonjwa kuonekana.Muuguzi pamoja na mwanamke mwingine wana ingia.

Julie. Tina, huyu ni Jayne, mmoja wa washaui hapa ,atakaa na sisi hapa leo, kama ni

sawa na wewe?

[Tina anakubali. Wote wana kaa chini.]

Julie. Sasa Tina tumekuja hapa leo ili yuongee juu ya matokea yako **[anasita].** matokeo yameonyesha yakwamba uko na chlamydia na hii inaweza tibiwa tutakupatia madawa hapa.

Tina. Hivyo ndivyo Graham alisema.....kwa hivyo inaweza tibiwa?

Julie. Ndio. **[anasita]** Lakini Tina, nina sitikika kukuambia damu yako ilionyesha uko na virusi vya Ukimwi **[Tina anashtuka]**

Jayne. Tina naelewa haukuwa unatarajia matokeo haya lakini ujue unaweza kututegemea hapa , unaweza anza madawa mara moja na kumbuka kuna watu wengi sana ambao wana virusi hivi na wanaishi maisha ya kawaida kila siku.

Tina ananyamaza.

Jayne. Nitaanza kukuona kutoka wiki hii na unaweza niambia kitu chochote kinacho kusumbua.

Julie. Pia naweza kukushauri na kukujibu maswali yoyote juu ya madawa ,hauko pekee yako Tina ,kuna mtu yeyote utapigia simu?

Tina anatingisha kichwa. Ana kaa kushtuka. mara anaanza kulia.

Jayne anamkumbatia.

ONYESHO LA NANE

Lafanyika kwenye ofisi ,Peter amekaa ,Simu yake inaanza kulia.

Peter. Habari?

Julie. Habari, naweza ongea na Peter Thompson tafadhali?

Peter. Ni yeye

Julie. Habari Peter. Mimi naitwa Julie, na mimi ni muuguzi huko wakefield kliniki ya GUM .Tunaweza kuongea?

Peter. Um…sawa ....nikusaidie na nini?

Julie. Peter, mmoja wa wapenzi wako alipimwa magonjwa ya zinaaa na matokea yakaonyesha kuwa ako nayo , ninakupigia simu ili nikueleze ni vizuri pia wewe upimwe ,

si lazima ukuje huku unaweza enda kliniki yeyote kupata matibabu.

Peter. Ngoja unasema niko na ugonjwa wa zinaa ... nani alikuja kukuona ? ilikuwa lini ?

Julie. Hatuwezi kukuambia ni nani alituambia lakini ni vizuri upimwe kwani ulifanya mapenzi bila kinga yeyote na nivizuri kujua

Peter. Sawa ,,,siamini hii , naweza kuja kliniki yenu ? Hauwezi niambia nini alipatikana nayo?

Julie. Ndiyo unaweza kuja hapa.Peter, unaweza kuwa na chlamydia lakini inaweza kutibiwa Pai unafaiwa kupimwa magonjwa yote ya zinaa sawa?unaweza kuja wiki hii? alamisi saa nne asubuhi?

Peter. Wiki hii ni sawa - alamisi saa nne ni sawa asante kwaheri. **[anamaliza kuongea na simu na anajiongelesha pekee yake].** Siamini! **[anajiambia]** Hii si bahati yangu - nilipoanza kuona wanawake wengine isipokua Helen na nina pata ugonjwa. **[anacheka]** wanaume wana wapenzi zaidi ya tano na hakuna magonjwa yanayowashika**[anasita]** labda naadhibiwa ...nasijui ni nani?**[anakunja sura akifikiria]** haiwezi kuwa Tina hana wanaume wengine isipokuwa mimi .....**[anasita]** lazima ni Gemma hajawai niambia alikuwa na wapenzi wangapi.

ONYESHO LA TISA

Lafanyika kwenye kliniki ya GUM.Peter ako kwenye chumba na Julie na Jayne

Peter. Pole lakini sielewi kile unachosema

Julie. Peter ,damu yako imepimwa na imeonekana kuwa na virusi vya ukimwi

Peter. [anakasirika] virusi vya ukimwi? Niko na virusi vya ukimwi?

Jayne. Tuna weza kukusaidia Peter kuna njia mingi ya kukabidhiana na ugonjwa huu . tuko hapa kukusaidia hautakuwa pekee yako.
Peter hasikizi na amewekelea mkono wake juu ya kichwa.

Peter [Bado mkono ko kichwani. Sauti yake inatoka polepole] Nataka kujua ni nani amenishikisha ugonjwa huu ,ni nani ameniambukiza ugonjwa huu? unaweza niambia ?

Julie. Ni vigumu kuseam kama haujakuwa na mpenzi mmoja , na kwasahii unafaiwa kujifikiria kufkiria maisha yako ya mbele ili kuwza kuishi maisha marefu na yenye afya.

Peter. anamwangalia] Siwzi fikiria hayo kwa sasa? Niko na bibi ? Na mtoto ! Bibi yangu ako na mimba !Nawezaji kukosa kufikiria juu ya mtu ambaye ameniharibia maisha

yangu yote?

Jayne. Najua ni ngumu lakini unafaiwa kutegemea familia yako wanaweza kukusaidia wakati huu **[anasita]** Najua si rahisi kufikiria maneneo haya kwa sasa lakini ni vizuri na muhimu umueleze mke wako aje kliniki kupimwa.

Uso wa Peter unakuwa nyejupe . Kwa kweli hakuwa amemfikiria mkewe.

Peter. Atakuwa …ata… anaweza kuwa na virusi ? Yaani anaweza kuwa na virusi tayari?

Julie. Anaweza kuwa hana virusi , lakini kwasababu mumekuwa mkifanya mapenzi ni muhimu apimwe pia na pia ni muhimu kwasababu ana mimba.

Peter. [anaangalia chini na kuweka mkono kichwani tena] Mungu wangu !!!

ONYESHO LA KUMI
Lafanyika kwenye jikoni ya nyumba ya Peter na Helen. Helen amekaa mezani anasoma kitabu, amewekelea mkono mmoja kwa tumbo lake ambalo linaonekana .Alex anacheza na kukimbia kwa nyumba.Peter anaingia mlangoni na mkoba wake.Nyuso lake ni nyeupe na anaonekana mwenye mawazo mengi.

Helen. [anaangalia juu] Habari mpenzi kazi ilikuwa aje? **[anamwangalia uso]** Peter? Nini mbaya mpenzi ?Hauonekani mzuri?

Helen anannza kuamka na Peter anamwambia akae. Peter anakaa chini kwa kiti kilichokuwa kando na kuweka mkoba chini.
Helen. [anaonekana mwenye wasiwasi] Peter,ni nini? Kuna kitu kimefanyika kazini ?Umepoteza kazi?

Peter. La sio kazi. **[anasita ,akitafuta la kumwambia].** Na … na taka kukuambia kitu Helen na .....an unafaiwa kusikiza Pole sana ...mungu wangu .... pole sana .

Kuna muziki [Gary Jules *Mad World*] inananza kuimba . Kwenye Onyesho hili hatusikii sauti ya waigizaji lakini tunawaona wakiongea .Peter anamwongelesha Helen akilia na kutingisha kichwa Helen anaonekana kushtuka na mkono wake unafunika mdomo ili asilie _ anatingisha kichwa kwa kutoamini na ana songa mbali na Peter. Anafunga macho , na machozi yana tiririka .Alex ana hisi kuna kitu mabaya anawacha kujimbia na kuwekelea mamake mkono.Helen anamwangali a na kumbeba ,anamwangalia Peter .Wote wanaangaliana bila kusema chochote.

MWISHO